**SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR**

**WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA AMALI**

# MUHUTASARI WA ELIMU YA MSINGI

# DARASA LA I – III

# MAZINGIRA

# 2022

© TEZ, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, 2022

Toleo la Kwanza 2022

Imesanifiwa na kuandaliwa na:

Taasisi ya Elimu ya Zanzibar (TEZ)

S.L.P 840,

Mazizini,

Zanzibar.

Barua Pepe: info@zie.go.tz

Tovuti: www.zie.go.tz

Simu: +255-24-2230193

ISBN:978-9912-754-19-5

Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kuiga, kunakili, kutafsiri, kupiga chapa au kutoa nyaraka hii kwa namna yoyote ile bila ya idhini ya Taasisi ya Elimu ya Zanzibar.

# YALIYOMO

DIBAJI............iv

SHUKURANI............v

1.0 UTANGULIZI............vi
1.1 Falsafa ya Elimu Zanzibar............vi
1.2 Madhumuni ya Elimu Zanzibar............vi
1.3 Malengo ya Elimu ya Msingi............vii
1.4 Sababu za Kupitia Mtaala wa Msingi............viii
1.5 Umuhimu wa Somo la Mazingira............viii
1.6 Matokeo ya Jumla ya Kujifunza Somo la Mazingira............viii

2.0 MUUNDO WA MUHUTASARI............ix
2.1 Kurasa za Awali............ix
2.2 Jaduweli la Ujifunzaji............ix
2.2.1 Mada............ix
2.2.2 Matokeo Mahususi ya kujifunza............ix
2.2.3 Mbinu za Kujifunzia............x
2.2.4 Nyenzo za kujifunzia............x
2.2.5 Upimaji............x
2.2.6 Vipindi............x
2.3 Mawanda na Mtiririko............xi

DARASA LA KWANZA............1

DARASA LA PILI............12

DARASA LA TATU............23

# DIBAJI

Muhutasari wa somo la Mazingira wa darasa la I-III wa mwaka 2022, unatokana na mabadiliko makubwa ya kielimu yaliyofanywa na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali (WEMA) ambayo yamehusisha kazi ya upitiaji wa Mtaala wa Elimu ya Maandalizi na Msingi ulioandikwa mwaka 2019. Madhumuni ya kupitia mtaala huo ni kuufanya uendane na maendeleo ya sayansi na teknolojia, ushindani wa soko la ajira pamoja na mabadiliko ya kiuchumi ulimwenguni kama inavyoelezwa katika nyaraka mbalimbali za Serikali ikiwemo Sera ya Elimu ya Zanzibar.

Kutokana na mabadiliko ya mfumo wa elimu Zanzibar, yaliyopelekea kurejeshwa kwa darasa la saba ikiwa ni miongoni mwa uimarishaji wa elimu ya Msingi, kwa sasa elimu ya Msingi itakuwa ni miaka 7 badala ya miaka 6 ya awali. Kwa kuzingatia mabadiliko hayo, WEMA kupitia Taasisi ya Elimu ya Zanzibar (TEZ) imeandika muhutasari wa somo la Mazingira ili kukidhi mahitaji ya taaluma hiyo. Kwa hivyo, muhutasari huu umekusanya mada za somo la Mazingira ambazo zinaendana na maudhui na muktadha wa somo hili. Kazi ya uandishi wa muhutasari huu imejumuisha wadau mbalimbali wa elimu katika ngazi tafauti hususan elimu ya Msingi. WEMA kupitia TEZ imehakikisha kuwa muhutasari umezingatia vyema maoni ya wadau hao, pamoja na mapitio ya machapisho mbalimbali kutoka nchi nyengine zinazofanana kijiografia, idadi ya wakaazi na mifumo ya elimu.

WEMA inatoa shukurani za dhati kwa wadau wote waliochangia katika kuandaa muhutasari huu wa somo la Mazingira wa darasa la I-III wakiwemo; Wajumbe wa Bodi ya Ushauri ya Taasisi, Uongozi na Watendaji wote wa TEZ, Jopo la Wataalamu, Wakuza Mitaala, Walimu na wastaafu mbalimbali wa WEMA walioshiriki katika matayarisho ya muhutasari huu hadi kukamilika kwake.

Ni matumaini ya WEMA kuwa, muhutasari huu utatumika kwa skuli zote za Zanzibar za Serikali na binafsi pamoja na watekelezaji wengine katika ngazi ya Elimu ya Msingi.

Khamis A. Said.
Katibu Mkuu,
Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali,
Zanzibar.

# SHUKURANI

Taasisi ya Elimu ya Zanzibar (TEZ) inatoa shukurani za dhati kwa Mh. Leila Muhamed Mussa, Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Mh. Ali Abdulghulam Hussein, Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, ndugu, Khamis Abdulla Said, Katibu Mkuu WEMA, Dkt. Mwanakhamis Adam Ameir Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar na Dkt. Abdullah Ismail Kanduru; Mwenyekiti wa Bodi ya Ushauri ya TEZ.

Shukurani za pekee ziwaendee wakuu wa divisheni za TEZ, wafanyakazi wote wa TEZ na Wajumbe wa Bodi ambao walikuwa ni washiriki wa kazi hii ya utayarishaji wa Muhutasari. Pia shukurani ziwaendee maafisa wa ngazi tafauti katika Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa kutumia muda wao na kutoa maoni kuhusu mambo yanayopaswa kuzingatiwa katika uandaaji wa muhutasari huu. Kwa kuongezea, TEZ inawashukuru walimu wote, wazazi na wanafunzi kwa kushiriki katika kazi hii.

Aidha, TEZ inazishukuru taasisi mbalimbali kwa kuwaruhusu watendaji wao kufanyakazi kwa pamoja. Taasisi zenyewe ni Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar, Chuo cha Abdulrahman Al-Sumait, Madrasa Early Childhood Programme Zanzibar (MECP-Z), Mamlaka ya Mji Mkongwe, Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi Zanzibar, Mamlaka ya Udhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya Zanzibar, Kitengo cha Elimu Mjumuisho na Stadi za Maisha, Hospitali ya Rufaa ya Mnazi Mmoja na Ofisi ya Mufti Mkuu Zanzibar. Taasisi nyengine ni Idara ya Mafunzo ya Ualimu, Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Elimu, Baraza la Mitihani la Zanzibar, Chuo cha Kiislamu, Idara ya Elimu ya Maandalizi na Msingi, Idara ya Elimu ya Sekondari, Jumuiya ya Skuli Binafsi na Taasisi nyengine zilizoshiriki katika kufanikisha upatikanaji wa Mihutasari ya Elimu ya Msingi.

TEZ inatoa shukurani za dhati kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na washirika wa maendeleo hususan Global Partnership for Education (GPE) kwa kutoa mchango wao wa hali na mali katika kukamilisha kazi hii.

Abdalla M. Mussa.
Mkurugenzi Mtendaji,
Taasisi ya Elimu ya Zanzibar,
Zanzibar.

# UTANGULIZI

Muhutasari wa somo la Mazingira umeandaliwa kwa wanafunzi wa darasa la I-III ambao umechukuwa nafasi ya somo la Sayansi Jamii na Sayansi yaliyokua yakifundishwa darasa la 1-IV kwa mtaala wa mwaka 2009. Muhutasari huu umejumuisha sehemu ya Utangulizi, Falsafa ya Elimu ya Zanzibar, Malengo na Madhumuni ya Elimu ya Zanzibar, Sababu za kupitiwa mtaala na umuhimu wa kujifunza somo la Mazingira. Pia, muhutasari huu umejumuisha Matokeo ya Jumla ya Kujifunza somo la Mazingira, Muundo wa Muhutasari, Matokeo ya Jumla ya Kujifunza kwa kila darasa pamoja na Jaduweli la Muhutasari.

## 1.1 Falsafa ya Elimu ya Zanzibar

Mfumo wa Mtaala wa Elimu ya Maandalizi na Msingi unakwenda sambamba na falsafa ya elimu ya Zanzibar, unaozingatia mila na misingi ya mfumo wa elimu hiyo.

Falsafa ya elimu ya Zanzibar ni sawa na ile ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambayo imejikita katika falsafa ya Ujamaa na Kujitegemea. Falsafa hii, inajumuisha kujitosheleza, kujiamini, uendelevu, kuwa na stadi za maisha, kuthamini usawa, ujasiriamali, uvumbuzi, udadisi, ubunifu na uwezo wa kutathmini na kuchambua.

## 1.2 Madhumuni ya Elimu ya Zanzibar

Yafuatayo ni madhumuni ya elimu Zanzibar:

1. Kukuza na kudumisha tabia na desturi bora za Wazanzibari na Watanzania ili kuimarisha umoja na utambulisho wao wa kiutamaduni.
2. Kuimarisha upatikanaji na matumizi sahihi ya aina mbalimbali za maarifa, stadi na mwelekeo/mwenendo kwa ajili ya kuendeleza kikamilifu utu na ubora wa maisha ya jamii.
3. Kumuwezesha kila mwananchi kuelewa na kuheshimu misingi ya Katiba ya Zanzibar na ya Tanzania, Haki za Binadamu, pamoja na haki, wajibu na majukumu ya kiraia.
4. Kuendeleza na kuhimiza matumizi bora, uangalizi na utunzaji wa mazingira.
5. Kukuza utashi na heshima ya kufanya kazi za kujiajiri na kuajiriwa pamoja na nidhamu kazini na utendaji kazi kwa kiwango cha juu cha ubora.
6. Kukuza na kudumisha misingi ya kuvumiliana, amani, upendo, haki, maelewano, haki za binadamu na uhuru, umoja wa kitaifa na kimataifa kama vinavyofafanuliwa katika mikataba ya kimataifa.

### 1.3 Malengo ya Elimu ya Msingi

Yafuatayo ni malengo ya Elimu ya Msingi Zanzibar:

1. Kuwezesha watoto wote wenye umri wa kwenda skuli kujenga na kudumisha misingi imara ya stadi za kusoma, kuandika, kuhesabu, kubuni na kuwasiliana kwa lugha za Kiswahili, Kiingereza na lugha nyengine za kigeni.
2. Kuwezesha wanafunzi kuelewa matumizi ya sayansi na teknolojia na kutambua mchango wake katika maendeleo ya kitaifa na kimataifa.
3. Kuweka, kuendeleza na kudumisha miongoni mwa wanafunzi misingi imara ya stadi za kufikiri na udadisi ili kuelewa mazingira yao na mahusiano ya kijamii.
4. Kuwezesha wanafunzi kuelewa jinsi matukio yaliyopita yanavyoathiri matukio ya wakati uliopo na ya wakati ujao.
5. Kugundua vipaji vya kila mwanafunzi kuanzia umri mdogo ili kuvidumisha na kuviendeleza.
6. Kuweka misingi imara ya stadi za uchunguzi, fikra na ushirikiano katika kutatua matatizo yanayodumaza maendeleo binafsi ya wanafunzi na ya jamii yao.
7. Kuwaandaa wanafunzi kujiunga na elimu ya sekondari.
8. Kuwezesha wanafunzi kukuza uwezo wao kiakili na utashi wa kujitafutia maarifa.
9. Kuwazoesha wanafunzi shughuli za uzalishaji mali na kukuza ari yao katika kutekeleza majukumu ya kijamii.
10. Kuwawezesha wanafunzi kutambua na kuenzi umoja wa taifa lao pamoja na ushirikiano baina ya taifa lao na watu wa mataifa mengine.
11. Kuwawezesha wanafunzi kujenga maadili mema kiroho, kiutamaduni na kiitikadi ili kukuza uzalendo na kufahamu hali ya nchi yao kihistoria, kisiasa na kijamii.
12. Kukuza na kudumisha nidhamu binafsi ya wanafunzi, kuheshimu usawa wa kijinsia na kulinda afya zao na za watu wengine.
13. Kuwawezesha wanafunzi kujenga tabia za umaridadi na unadhifu pamoja na matumizi bora ya muda wao wa mapumziko.
14. Kukuza upendo wa wanafunzi katika mazingira wanamoishi pamoja na utashi wa kuyatunza.

### 1.4 Sababu za Kupitiwa Mtaala wa Elimu ya Msingi

Mnamo mwaka 2019, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ilifanya mapitio ya Mtaala wa Elimu ya Maandalizi na Msingi. Madhumuni yalikuwa ni kuufanya mtaala uendane na maendeleo ya sayansi na teknolojia, ushindani wa soko la ajira na mabadiliko ya kiuchumi ulimwenguni kama inavyoelezwa katika nyaraka mbalimbali za Serikali ikiwemo Sera ya Elimu ya Zanzibar. Sera hiyo inalenga kuimarisha ubora na muundo wa elimu ili kuwa na muunganiko mzuri unaoanzia Elimu ya Maandalizi, Msingi na Sekondari ili kukidhi matarajio ya walengwa na jamii yao. Miongoni mwa mabadiliko yaliyopendekezwa ni kuwa na miaka saba (7) ya elimu ya msingi badala ya miaka sita (6) ya awali.

### 1.5 Umuhimu wa Kujifunza Somo la Mazingira

Katika mapitio yaliyofanywa mwaka 2019 ilibainika kwamba somo la Mazingira halikuwa ni lenye kujitegemea bali ilikuwa ni miongoni mwa mada zilizomo katika somo la Sayansi jamii na Sayansi lilianzia darasa la I – VI. Hivyo, kutokana na mahitaji ya jamii, imeonekana ni vyema somo la Mazingira liweze kujitegemea kuanzia darasa la I -III. Hii ni kutokana kuwa, Somo hili humsaidia mwanafunzi kumjengea maarifa, stadi na mwelekeo chanya wa kumuwezesha kutunza na kuthamini mazingira yake yaliyomzunguka. Pia, somo la Mazingira linamsaidia mwanafunzi kuimarisha afya yake na kuweza kujikinga na magonjwa ya kuambukiza na yasiyoambukiza. Zaidi, somo hili linamsaidia mwanafunzi katika kuendeleza utamaduni wa mzanzibari, kuwa raia mwema na kubuni shughuli zitakazomwezesha kujitegemea.

### 1.6 Matokeo ya Jumla ya Kujifunza Somo la Mazingira

Baada ya kusoma somo la Mazingira katika skuli za msingi, wanafunzi wataonesha ujuzi wa: -

1. Kuelewa taratibu za afya, kujiheshimu na kujitunza, usafi wa mwili pamoja na mazingira, Kwa mfano; kutambua ugonjwa maarufu na sababu zake, kuainisha sehemu za mwili na kazi zake na kadhalika.
2. Kutambua maumbile ya mazingira yao na kufahamu mambo yanayoyaathiri, Kwa mfano; kutambua maeneo mbalimbali ya kiuchumi ya Zanzibar na sifa zake, kutambua kufanana na kutafautiana kwa wanyama, kuthamini umuhimu wa kutumia rasilimali kwa njia sahihi na kadhalika
3. Kuheshimu haki za binaadamu pamoja na kuwa na ustahamilivu wa kiutamaduni na kidini

4. Kukusanya taarifa, maarifa na ujuzi kutoka vyanzo mbalimbali vya TEHAMA na kuzitumia ipasavyo kwa maendeleo ya mtu binafsi na kijamii kwa ujumla
5. Kuelewa haki na wajibu wao, katika familia, jamii na nchi yao.
6. Kufahamu na kuthamini historia ya Zanzibar na za nchi jirani.

## 2.0 MUUNDO WA MUHUTASARI

Muhutasari huu una sehemu kuu mbili: Kurasa za awali na Jaduweli la Muhutasari.

### 2.1 Kurasa za Awali

Sehemu hii inajumuisha utangulizi wa Muhutasari, Falsafa ya Elimu ya Zanzibar, Malengo ya Elimu ya Msingi Zanzibar, pamoja na umuhimu wa kujifunza somo la Mazingira. Pia, kuna matokeo ya jumla ya kujifunza somo hili. Vipengele vyengine ni; maelezo kuhusu mawanda na mtiririko wa mada zilizomo, matokeo ya jumla ya darasa husika na ufafanuzi wa vipengele vya jaduweli la ujifunzaji.

### 2.2 Jaduweli la Ujifunzaji

Sehemu hii inaonesha utaratibu wa ujifunzaji uliobainishwa katika majadweli matatu yaliyobeba maudhui ya darasa la I hadi la III. Kila jaduweli limeanza na orodha ya matokeo ya jumla ya kujifunza kwa darasa linalohusika. Baada ya matokeo ya jumla linafuata jadweli la ujifunzaji lenye safuwima sita zenye Mada, Matokeo Mahususi ya Kujifunza, Mbinu za Kujifunzia, Nyenzo za Kujifunzia, Upimaji na Vipindi kwa kila mada ndogo. Yafuatayo ni maelezo ya kila kipengele.

#### 2.2.1 Mada

Mada zimejikita katika mawanda ya ufundishaji na ujifunzaji wa mada husika.

#### 2.2.2 Matokeo Mahususi ya Kujifunza

Kila mada ndogo huonesha matokeo mahususi ya kujifunza. Matokeo hayo yanaelezea maarifa, ujuzi na mwelekeo ambao kila mwanafunzi anapaswa kujifunza katika mada ndogo inayohusika. Matokeo mahususi ndiyo yanayotumiwa kufanyia upimaji, ambayo hudokeza viashiria vinavyojenga umahiri. Kwa kawaida, wakati wa kujifunza mwanafunzi huanza kuonesha viashiria hivyo akiwa darasani. Hivyo kila mwanafunzi anatakiwa kuyafikia matokeo mahususi yaliyotajwa.

### 2.2.3 Mbinu za Kujifunzia

Safuwima hii imejumuisha mbinu shirikishi za kutumia katika kujifunzia mada za somo hili. Mbinu hizo ni kama; maswali na majibu, bungua bongo, onesho mbinu, igizo dhima, uvumbuzi, matembezi ukumbini, fikiri jozisha shirikisha, majadiliano na mazoezi ya vitendo. Haya ni mapendekezo ya mbinu ambazo zimethibitika kuongeza ushiriki wa wanafunzi katika vitendo vya kujifunza. Mwalimu anashauriwa kutumia mbinu nyengine shirikishi atakazoona zinafaa kufundishia kulingana na mazingira yake.

### 2.2.4 Nyenzo za Kujifunzia

Nyenzo za kujifunzia huendana na mbinu za kujifunzia, matokeo mahususi ya kujifunza, mada ndogo na mahitaji ya kila mada ndogo. Hata hivyo, nyenzo zilizoorodheshwa ni mapendekezo tu, mwalimu anashauriwa kuwa mbunifu katika kutengeneza nyenzo zinazotokana na mazingira halisi au malighafi za bei nafuu. Aidha, mwalimu ashirikiane na wanafunzi kubuni na kutengeneza zana za kujifunzia kwa kutumia malighafi zilizomo katika mazingira yao.

### 2.2.5 Upimaji

Katika safuwima hii, zimependekezwa njia za kupima iwapo mwanafunzi amefikia matokeo mahususi ya kujifunza kwa mada husika. Kila siku, wiki, mwezi, muhula na mwisho wa mwaka wa masomo mwalimu anahimizwa kupima maendeleo ya kila mwanafunzi kwa kutumia njia mbalimbali. Njia hizo za upimaji ni kama vile upimaji binafsi, uchunguzi, mkoba wa kazi, orodha hakiki, maswali na majibu na mazoezi. Wakati wa kuzitumia njia hizo, ni vyema mwalimu akazingatia mapendekezo ya upimaji yaliyomo katika muhutasari pamoja na kuzingatia mahitaji ya kila mwanafunzi.

### 2.2.6 Vipindi

Hii ni safu-wima inayoonesha idadi ya vipindi kwa mada zinazofundishwa. Idadi hiyo imefikiwa baada ya kujumlisha vipindi vya somo hili kwa mwaka wa masomo (siku 210) kwa kila darasa. Jumla hiyo imegawika kwa idadi ya mada ndogo zilizomo katika muhutasari ili kupata wastani wa vipindi kwa kila mada ndogo. Makadirio haya yanaweza kubadilishwa na mwalimu kulingana na mazingira ya ujifunzaji wa mada husika. Somo la Mazingira lina vipindi (6) kwa wiki kwa darasa la I na la II na vipindi (7) kwa wiki kwa darasa la III.

Kuanzia Jumatatu hadi Alhamisi muda wa kipindi kimoja ni dakika arobaini (40) kwa mkondo wa asubuhi, dakika thelathini na tano (35) kwa mkondo wa mchana.

Siku ya Ijumaa kila kipindi kitachukua dakika thelathini (30) tu. Utawala wa skuli unahimizwa kufidia muda wa masomo utakaopotea kutokana na dharura za sikukuu za kidini au za kiserikali.

## 2.3 Mawanda na Mtiririko

Mada zimepangwa kulingana na makuzi ya wanafunzi ya kiakili, kiroho, kimwili na kihisia. Pia uwezo wao wa kujifunza, umuhimu wa somo katika shughuli za kiuchumi katika jamii yao na kutegemeana kwa mada. Aidha, mada za masuala mtambuka, hususan ujasiriamali na stadi za maisha zimezingatiwa.

Mwalimu anashauriwa kufundisha mada hizi kwa kuzingatia mazingira ya kujifunzia na muktadha utakaofaa. Jaduweli lifuatalo linaonesha mpangilio wa mada zilizopendekezwa katika Muhutasari:

| NA. | MPANGILIO WA MADA KWA DARASA | | | |
|---|---|---|---|---|
| | MADA | DARASA LA I | DARASA LA II | DARASA LA III |
| 1. | USAFI | √ | √ | |
| 2. | MAZINGIRA YETU | √ | √ | √ |
| 3. | TAKA | | | √ |
| 4. | CHAKULA NA LISHE | √ | √ | √ |
| 5. | MARADHI | | | √ |
| 6. | HUDUMA YA KWANZA | | | √ |
| 7. | WANYAMA | √ | √ | √ |
| 8. | UTAMADUNI WETU | √ | √ | |
| 9. | MAADILI YETU | √ | √ | √ |
| 10. | UCHUMI WETU | | | √ |
| 11. | MAWASILIANO | √ | √ | √ |
| **JUMLA** | | **7** | **7** | **9** |

# DARASA I

## DARASA LA I

### Matokeo ya Jumla ya Kujifunza kwa Darasa la Kwanza

Katika kujifunza somo la Mazingira kwa darasa la kwanza mwanafunzi aoneshe uwezo wa:

1. Kudumisha usafi wa mwili na mavazi katika maisha ya kila siku.
2. Kutumia maji safi na salama na kuhifadhi vyanzo vyake.
3. Kutambua makundi ya vyakula katika kujenga na kulinda afya.
4. Kutambua umuhimu wa wanyama wanaofugwa na wasiofugwa katika kunyanyua uchumi wa Taifa.
5. Kutambua na kuendeleza shughuli za utamaduni na kujenga uthubutu.
6. Kutambua na kutekeleza misingi ya maadili yanayokubalika katika jamii.
7. Kutambua na kutumia mawasiliano katika kupata maarifa na stadi za kisayansi.

## DARASA LA KWANZA

| MADA | MATOKEO MAHUSUSI YA KUJIFUNZA | MBINU ZA KUJIFUNZIA | NYENZO ZA KUJIFUNZIA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|
| **1. USAFI**<br><br>1.1 Usafi wa Mwili | **Mwanafunzi aoneshe uwezo wa:**<br>i. Kubainisha vifaa vya kufanyia usafi wa mwili.<br>ii. Kuelezea utaratibu wa kusafisha mwili.<br>iii. Kuelezea faida za usafi wa mwili.<br>iv. Kujadili hasara za kutokufanya usafi wa mwili. | • Maswali na majibu<br>• Nyimbo<br>• Hadithi<br>• Maigizo<br>• Majigambo<br>• Majadiliano<br>• Matembezi ukumbini<br>• Onesho mbinu<br>• Uwasilishaji kwa TEHAMA | • Sabuni<br>• Kitana<br>• Ndoo<br>• Miswaki<br>• Mashanuo<br>• Dawa ya meno<br>• Taula<br>• Kiwembe cha kukatia kucha<br>• Maji<br>• Mafuta<br>• Chati zinazoonesha vifaa vya usafi wa mwili<br>• Video zinaoonesha usafi wa mwili<br>• Flashi/CD<br>• Kompyuta<br>• Projekta<br>• shampuu | • Maswali na majibu<br>• Majadiliano<br>• Usahihishajirika<br>• Orodha hakiki<br>• Mkoba wa kazi | 18 |

| MADA | MATOKEO MAHUSUSI YA KUJIFUNZA | MBINU ZA KUJIFUNZIA | NYENZO ZA KUJIFUNZIA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|
| 1.2 Usafi wa Mavazi | **Mwanafunzi aoneshe uwezo wa:**<br>i. Kuainisha vifaa vya kufanyia usafi wa mavazi.<br>ii. Kuelezea hatua katika kufanya usafi wa mavazi.<br>iii. Kujadili faida za usafi wa mavazi. | • Bungua bongo<br>• Majadiliano<br>• Matembezi ukumbini<br>• Onesho mbinu<br>• Maswali na majibu<br>• Kisa mafunzo<br>• Uwasilishaji kwa TEHAMA | • Sabuni<br>• Maji<br>• Ndoo<br>• Vibanio<br>• Kamba za kuanikia nguo<br>• Pasi<br>• Brashi<br>• Nguo mbali mbali<br>• Chati zinazoonesha vifaa vya usafi wa mavazi<br>• Video inaoonesha usafi wa mavazi<br>• Flashi/DVD<br>• Televisheni Kompyuta<br>• Projekta<br>• Henga | • Kadi mrejesho<br>• Maswali na majibu<br>• Majadiliano<br>• Uchunguzi<br>• Orodha hakiki | 18 |
| **2. MAZINGIRA YETU**<br>2.1 Maji | **Mwanafunzi aoneshe uwezo wa:**<br>i. Kuelezea maji safi na salama. | • Bungua bongo<br>• Maswali na majibu<br>• Majadiliano<br>• Onesho mbinu | • Picha zinazoonesha matumizi ya maji<br>• Vipeperushi<br>• Flashi/DVD | • Maswali na majibu<br>• Majadiliano<br>• Kazi mradi<br>• Utafiti | 18 |

| MADA | MATOKEO MAHUSUSI YA KUJIFUNZA | MBINU ZA KUJIFUNZIA | NYENZO ZA KUJIFUNZIA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|
| | ii. Kujadili matumizi ya maji.<br>iii. Kufafanua madhara yanayotokana na maji yasio safi na salama. | • Uchunguzi<br>• Uwasilishaji kwa TEHAMA | • Televisheni<br>• Kompyuta<br>• Projekta | • Orodha hakiki<br>• Mkoba wa kazi | |
| 2.2 Vyanzo vya Maji | **Mwanafunzi aoneshe uwezo wa:**<br>i. Kuainisha vyanzo vya maji.<br>ii. Kuelezea njia za kuhifadhi vyanzo vya maji.<br>iii. Kufafanua faida za kuhifadhi vyanzo vya maji.<br>iv. Kuelezea madhara ya kuharibu vyanzo vya maji. | • Bungua bongo<br>• Majadiliano<br>• Ziara za kimasomo<br>• Onesho mbinu<br>• Maswali na majibu<br>• Chemsha bongo<br>• Uwasilishaji kwa TEHAMA<br>• Kumualika mgeni | • Picha za vyanzo vya maji (Maji ya bahari maziwa, mito, kisima, chemchem, mifereji, mvua)<br>• Video zinazoonesha vyanzo vya maji<br>• Flashi/DVD<br>• Televisheni<br>• Kinasa sauti<br>• Kompyuta<br>• Projekta | • Kujisahihisha<br>• Majadiliano<br>• Utafiti | 18 |
| **3. CHAKULA NA LISHE** | **Mwanafunzi aoneshe uwezo wa:**<br>i. Kuainisha makundi ya vyakula. | • Nyimbo<br>• Fikiri jozisha shirikisha<br>• Majadiliano | • Vyakula halisi vya uwanga mafuta, protini, madini, vitamini | • Kadi ya kutoka<br>• Maswali na majibu<br>• Majadiliano | 18 |

| MADA | MATOKEO MAHUSUSI YA KUJIFUNZA | MBINU ZA KUJIFUNZIA | NYENZO ZA KUJIFUNZIA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|
| 3.1 Makundi ya Vyakula | ii. Kuelezea faida za makundi ya vyakula. | • Kisa mafunzo<br>• Ziara za kimasomo<br>• Maswali na majibu<br>• Majigambo<br>• Michezo<br>• Uwasilishaji kwa TEHAMA | • Picha za vyakula<br>• Modeli za vyakula<br>• Chati za makundi ya vyakula<br>• Flashi/DVD<br>• Televisheni<br>• Kompyuta<br>• Projekta | • Kazi mradi<br>• Uchunguzi<br>• Orodha hakiki | |
| 3.2 Usafi na Usalama wa Chakula | **Mwanafunzi aoneshe uwezo wa:**<br>i. Kubainisha mambo muhimu ya kuzingatia katika usafi na usalama wa chakula.<br>ii. Kuelezea faida za usafi na usalama wa chakula.<br>iii. Kufafanua njia bora za kuhifadhi chakula katika hali ya usafi na usalama. | • Maswali na majibu<br>• Igizo dhima<br>• Onesho mbinu<br>• Ziara za kimasomo<br>• Nyimbo<br>• Kisa mafunzo<br>• Uwasilishaji kwa TEHAMA | • Kawa<br>• Picha ya kabati<br>• Picha ya friji<br>• Picha ya sanduku la kuhifadhia chakula<br>• Vipeperushi<br>• Chati za vyakula<br>• Kompyuta<br>• Projekta<br>• Video zinazoonesha usafi na usalama wa chakula | • Tathmini binafsi<br>• Maswali na majibu<br>• Majadiliano<br>• Mkoba wa kazi | 18 |

| MADA | MATOKEO MAHUSUSI YA KUJIFUNZA | MBINU ZA KUJIFUNZIA | NYENZO ZA KUJIFUNZIA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|
| **4. WANYAMA**<br><br>4.1 Wanyama Wanaofugwa | **Mwanafunzi aoneshe uwezo wa:**<br>i. Kuainisha wanyama wanaofugwa.<br>ii. Kuelezea faida za wanyama wanaofugwa. | • Maswali na majibu<br>• Nyimbo<br>• Hadithi<br>• Michezo<br>• Fikiri jozisha shirikisha<br>• Kisa mafunzo<br>• Majigambo<br>• Majadiliano<br>• Matembezi ukumbini<br>• Uwasilishaji kwa TEHAMA | • Picha za wanyama wanaofugwa<br>• Video za wanyama wanaofugwa<br>• Kompyuta<br>• Flashi/DVD<br>• Televisheni<br>• Projekta<br>• Modeli za Wanyama wanaofugwa | • Kadi mrejesho<br>• Majadiliano<br>• Kazi mradi<br>• Uchunguzi | 18 |
| 4.2 Wanyama Wasiofugwa | **Mwanafunzi aoneshe uwezo wa:**<br>i. Kuainisha wanyama wasiofugwa.<br>ii. Kuelezea faida za wanyama wasiofugwa. | • Vitendawili<br>• Maswali na majibu<br>• Nyimbo<br>• Hadithi<br>• Kisa mafunzo<br>• Majadiliano<br>• Ziara ya kimasomo<br>• Michezo | • Chati za wanyama wasiofugwa<br>• Modeli za Wanyama wasiofugwa<br>• Video zinazoonesha wanyama wasiofugwa<br>• Flashi/DVD<br>• Televisheni | • Maswali na majibu<br>• Majadiliano<br>• Uchunguzi | 18 |

| MADA | MATOKEO MAHUSUSI YA KUJIFUNZA | MBINU ZA KUJIFUNZIA | NYENZO ZA KUJIFUNZIA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|
| | | • Matembezi ukumbini<br>• Uwasilishaji kwa TEHAMA | • Kinasa sauti<br>• Kompyuta<br>• Projekta | | |
| **5. UTAMADUNI WETU**<br><br>5.1 Matukio ya Kiutamaduni | **Mwanafunzi aoneshe uwezo wa:**<br>i. Kuanisha vipengele vya utamaduni.<br>ii. Kuelezea matukio ya kiutamaduni katika jamii.<br>iii. Kujadili umuhimu wa matukio ya kiutamaduni katika jamii. | • Bungua bongo<br>• Majadiliano<br>• Maswali na majibu<br>• Hadithi<br>• Majigambo<br>• Uwasilishaji kwa TEHAMA | • Kadi za vipengele vya utamaduni<br>• Picha za matukio ya kiutamaduni<br>• Flashi/DVD<br>• Televisheni<br>• Projekta<br>• Kompyuta<br>• Video zinazoonesha matukio ya kiutamaduni | • Maswali na majibu<br>• Majadiliano<br>• Orodha hakiki<br>• Uchunguzi<br>• Mkoba wa kazi | 18 |
| 5.2 Uthubutu | **Mwanafunzi aoneshe uwezo wa:**<br>i. Kuelezea dhana ya uthubutu.<br>ii. Kufafanua njia za kukuza uthubutu kwa watoto. | • Bungua bongo<br>• Maswali na majibu<br>• Masimulizi<br>• Nyimbo<br>• Chemsha bongo<br>• Majadiliano<br>• Kualika mgeni<br>• Igizo dhima | • Kinasa sauti<br>• Redio<br>• Televisheni<br>• Flashi/DVD<br>• Vipeperushi<br>• Kompyuta<br>• Projekta | • Tathmini binafsi<br>• Majadiliano<br>• Usahihishaji rika | 18 |

| MADA | MATOKEO MAHUSUSI YA KUJIFUNZA | MBINU ZA KUJIFUNZIA | NYENZO ZA KUJIFUNZIA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|
| | iii. Kujadili faida za kuwa na uthubutu.<br>iv. Kufafanua madhara ya kukosa uthubutu kwa watoto. | • Kisa mafunzo<br>• Michezo<br>• Uwasilishaji kwa TEHAMA | | | |
| **6. MAADILI YETU**<br><br>6.1 Dhana ya Maadili | **Mwanafunzi aoneshe uwezo wa:**<br>i. Kuainisha vitendo vinavyoashiria maadili.<br>ii. Kuelezea faida za kuwa na maadili katika jamii.<br>iii. Kujadili madhara ya kutokuwa na maadili katika jamii. | • Bungua bongo<br>• Nyimbo<br>• Majadiliano<br>• Maswali na majibu<br>• Maigizo<br>• Kisa mafunzo<br>• Uwasilishaji kwa TEHAMA | • Vipeperushi<br>• Flashi/DVD<br>• Televisheni<br>• Kompyuta<br>• Projekta<br>• Kinasa sauti | • Dole gumba juu dole gumba chini<br>• Majadiliano<br>• Maswali ya papo kwa papo | 18 |
| 6.2 Misingi ya Maadili | **Mwanafunzi aoneshe uwezo wa:**<br>i. Kubainisha misingi ya maadili.<br>ii. Kufafanua vyanzo vya misingi ya maadili.<br>iii. Kueleza namna ya kutekeleza maadili. | • Bungua bongo<br>• Majadiliano<br>• Maswali na majibu<br>• Maigizo<br>• Kisa mafunzo<br>• Uwasilishaji kwa TEHAMA<br>• Kumualika mgeni | • Vipeperushi<br>• Flashi/DVD<br>• Televisheni<br>• Kompyuta<br>• Projekta | • Majadiliano<br>• Tathmini binafsi<br>• Uchunguzi<br>• Mkoba wa kazi | 18 |

| MADA | MATOKEO MAHUSUSI YA KUJIFUNZA | MBINU ZA KUJIFUNZIA | NYENZO ZA KUJIFUNZIA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|
| **7. MAWASILIANO**<br><br>7.1 Dhana ya Mawasiliano | **Mwanafunzi aoneshe uwezo wa:**<br><br>i. Kuainisha vifaa vya mawasiliano.<br>ii. Kuelezea umuhimu wa mawasiliano. | • Maswali na majibu<br>• Bungua bongo<br>• Onesho mbinu<br>• Majadiliano<br>• Fikiri jozisha shirikisha<br>• Majigambo<br>• Uwasilishaji kwa TEHAMA<br>• Ziara ya kimasomo | • Televisheni<br>• Redio<br>• Simu<br>• Ngoma<br>• Zumari<br>• Filimbi<br>• Upatu<br>• Kompyuta<br>• Projekta<br>• Chati za vifaa vya mawasiliano<br>• Barua<br>• Magazeti<br>• Vipeperushi<br>• Zumari<br>• Video zinazoenesha mawasiliano<br>• Flashi/DVD | • Majadiliano<br>• Orodha hakiki<br>• Maswali na majibu<br>• Kadi mrejesho<br>• Mkoba wa kazi | 18 |
| 7.2 Mawasiliano ya Alama (barabarani, skuli, hospitali, | **Mwanafunzi aoneshe uwezo wa:**<br><br>i. Kubainisha alama za mawasiliano. | • Maswali na majibu<br>• Matembezi ukumbini<br>• Onesho mbinu<br>• Majadiliano | • Televisheni<br>• Kompyuta<br>• Chati zinazoonesha mawasiliano ya alama | • Dole gumba juu dole gumba chini<br>• Utafiti<br>• Orodha hakiki<br>• Uchunguzi | 18 |

| MADA | MATOKEO MAHUSUSI YA KUJIFUNZA | MBINU ZA KUJIFUNZIA | NYENZO ZA KUJIFUNZIA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|
| nyumba za ibada) | ii. Kuelezea matumizi ya alama za mawasiliano. | | • Vipeperushi<br>• Projekta<br>• Picha zinazoonesha mawasiliano ya alama<br>• Kinasa sauti | • Mkoba wa kazi | |

# DARASA II

## DARASA LA II

### Matokeo ya Jumla ya Kujifunza kwa Darasa la Pili

Katika kujifunza somo la Mazingira kwa darasa la pili, mwanafunzi aoneshe uwezo wa:

1. Kupenda na kusafisha mazingira.
2. Kuhifadhi mazingira na kujiepusha na vitendo vinavyoharibu mazingira.
3. Kutumia vyakula bora ili kujenga na kulinda afya ya mwili.
4. Kutambua umuhimu wa wanyama wanaoishi nchi kavu na kwenye maji ili kunyanyua uchumi wa Taifa.
5. Kutambua na kuendeleza urithi wa utamaduni wa Mzanzibari.
6. Kujiepusha na vitendo vinavyopelekea mmong'onyoko wa maadili.
7. Kutumia mawasiliano ya kisasa na ya kale ili kupata maarifa na stadi za kisayansi.

## DARASA LA PILI

| MADA | MATOKEO MAHUSUSI YA KUJIFUNZA | MBINU ZA KUJIFUNZIA | NYENZO ZA KUJIFUNZIA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|
